HelpAge International
age helps

# Haki za Binadamu na Taratibu za Mahakama

## Kitini cha Wazee washauri vijijini



BMZ
Federal Ministry
for Economic Cooperation
and Development

HelpAge Deutschland
Alter ist Zukunft

## UTANGULIZI:

Kitini hiki cha Wazee washauri kimetengenezwa kama sehemu ya mradi wa miaka mitatu wa ''***Kulinda na kuwaenzi wanawake wazee na kuwawezesha kijamii na kiutamaduni nchini Tanzania''.*** Mradi huu unalenga kuboresha haki za Wazee (hasa Wazee wanawake) kwa kuwawezesha kupitia shughuli mbali mbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa ushauri, kusikiliza malalamiko, na kutoa ushauri nasaha na maelekezo yenye misingi ya kisheria pale inapobidi.

Mradi huu utatekelezwa na shirika la Magu Poverty Eradication Centre (MAPERECE) katika kata nne za Wilaya ya Magu na Kwimba; na Shirika la Saidia Wazee Karagwe (SAWAKA) kwenye kata nne za Wilaya ya Karagwe na Kyerwa. Pia mradi huu unatekeleza mojawapo ya vipaumbele vya Shirika la HelpAge International vya kuwawezesha Wazee wanawake na wanaume kupinga ubaguzi kiumri na kudai haki zao.

Kitini hiki kimetengenezwa ili kitumiwe na watu wenye umri mkubwa na kimeandikwa kwa lugha rahisi ili kuwezesha kuwepo kwa mijadala kati ya wanawake Wazee washauri waliopata mafunzo na Wazee watakaohitaji msaada wa kisheria. Maelezo yaliyomo katika kitini hiki yameandikwa kutoka katika haki za binadamu na taratibu za mahakama Tanzania kwa vile sehemu kubwa ya sheria hizi zinahusu masuala ambayo ni ya msingi kwa watu wa aina zote.

Watumiaji wa kitini hiki hasa wanatarajiwa kuwa ni Wazee washauri waliopata mafunzo pamoja na Wazee wengine kwa ujumla. Juhudi za makusudi zimefanyika kuhakikisha kuwa maandishi haya na lugha iliyotumika ni rafiki na imezingatia umri, jinsi, maoni, imani na viwango vya elimu na kwa watu wanaoishi vijijini. Lengo kuu la kitini hiki ni kuwapatia Wazee taarifa rahisi na sahihi za kuwawezesha kutambua masuala yanayoweza kusuluhishwa kwa amani kwa kutumia mbinu za kienyeji na yale yanayohitaji msaada wa kitaalamu wa kisheria. Kwa hali yoyote ile kitini hiki hakilengi kuwafanya Wazee washauri kudai kuwa wao ni wananasheria ama mawakili, na kwa vyovyote vile hakikutengenezwa kuchukua nafasi ya shughuli za wanasheria ama mawakili waliosomea taaluma hiyo. Kitini kinalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa rahisi na sahihi ili watu wafanye maamuzi ya busara juu ya hatua za kuchukua, na kuepuka migogoro ya muda mrefu na isiyo ya lazima wakati mawazo yaliyo kwenye kitini hiki yangeweza kutoa mwongozo. Tunaamini kuwa taarifa zilizo kwenye kitini hiki zitakuwa na manufaa kwa Wazee na wanajamii wengine wanaohitaji taarifa kuhusu haki za binadamu na taratibu za mahakama Tanzania.

# KUHUSU SISI

HelpAge International ni mtandao wa kimataifa wenye njozi ya kuwa na dunia ambamo Wazee wataishi maisha yenye hadhi, afya na nguvu .Lengo letu ni kuhakikisha kuwa wazee katika nchi ya Tanzania wanapata fursa sawa ya kutumia rasilimali na huduma kama ilivyobainishwa kwenye sera mbali mbali na mifumo ya sheria kwa kuingiza masuala ya Wazee katika mipango ya maendeleo ya nchi hii, na kuondoa umaskini unaowaathiri Wazee na wategemezi wao.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo;

HelpAge International Tanzania
134 Migombani Street
Regent Estate, Mikocheni
P. O. Box 9846
Dar es Salaam
Tanzania
Email: haitz@helpagetz.org

Magu Poverty Eradication Centre
P. O. Box 333
Magu
Tanzania
Email: maperece@hotmail.com

Saidia Wazee Karagwe
P.O.Box 21
Karagwe
Tanzania
Email: kasawatakaragwe@yahoo.com

## SHUKRANI

Utengenezwaji wa kitini hiki umewezeshwa kupitia msaada wa Wizara ya Ushirika wa Uchumi na Maendeleo ya Shirikisho la Ujerumani, HelpAge Germany na HelpAge International.

# YALIYOMO

1.0 Haki za binadamu........................................................................................ 4
1.1 Historia ya haki za binadamu na mikataba ya kimataifa.............................. 4
1.2 Nchi yetu na mikataba ya kimataifa.............................................................. 4
1.3 Haki za msingi za binadamu.......................................................................... 4
1.4 Haki za makundi maalumu............................................................................. 6
1.5 Haki za msingi za Wazee................................................................................ 7
1.6 Sheria na haki za binadamu.......................................................................... 8

1.7 Mahakama za Tanzania ................................................................................ 9
1.8 Mfumo wa mahakama za Tanzania............................................................... 9
1.8.1 Mahakama za mwanzo.................................................................... 9
1.8.2 Mahakama za wilaya....................................................................... 10
1.8.3 Mahakama za hakimu mkazi.......................................................... 10
1.8.4 Mahakama kuu ya Tanzania........................................................... 10
1.8.5 Mahakama ya rufaa ya Tanzania.................................................... 11

2.0 Taratibu za mahakama................................................................................... 12
2.1 Kesi za madai............................................................................................ 12
2.2 Kesi za jinai .............................................................................................. 13

3.0 Sheria ya ushahidi mahakamani.................................................................... 15
3.1 Aina za ushahidi........................................................................................ 15
3.2 Nani anaweza kutoa ushahidi.................................................................. 15
3.3 Ushahidi unaokubalika mahakamani....................................................... 17

4.0 Rufaa.................................................................................................................. 18
4.1 Mwenendo wa rufaa..................................................................................... 18

5.0 Dhamana........................................................................................................... 19

# HAKI ZA BINADAMU

## Maana ya haki

Haki ni stahili aliyonayo mtu, kwa kuzaliwa au kupewa katika dunia hii ili aweze kuishi na kufurahia maisha yake". Stahili hii mara zote huenda sambamba na utimizwaji wa wajibu au majukumu ya mhusika. Wajibu huu ni pamoja na kupendana, kuheshimiana, kuthaminiana, kutonyanyasana au kubaguana kwa njia yoyote ile.

## Historia ya haki za binadamu na mikataba ya kimataifa

Masuala ya Haki za Binadamu yalianza baada ya vita kuu za dunia I na II vilivyopelekea kuwepo uvunjwaji mkubwa wa haki za binadamu. Vita hizo zilisababisha mateka wa kivita ambao walikuwa wakitendewa ukatili. Pia madhara yake yalikuwa ni pamoja na watu kupata ulemavu wa kudumu, wajane na yatima wengi walitokana na vita hivyo.

Hali kadhalika zilikuwepo mila potofu zilizowafupishia maisha watoto waliozaliwa na ulemavu wa viungo au upungufu wa rangi ya ngozi.

Mwaka 1948 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha tamko la "Haki za Binadamu". Pamoja na mambo mengine, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, ikizingatiwa kuwa zimethibitisha imani yake katika haki za kimsingi za binadamu, heshima, thamani ya mtu na haki sawa kwa wote, zimetunga mikataba na kutoa matamko na maazimio mbalimbali.

## Nchi yetu na mikataba ya kimataifa

Tanzania ikiwa kama mwanachama wa Umoja Wa Mataifa imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa na kusaini maazimio na matamko yanayohusiana na haki za binadamu kimataifa.

Ni wajibu wa kila nchi inayoridhia na kusaini mikataba hiyo ya kimataifa kuiingiza mikataba ya kimataifa katika sheria zake za nchi. Mwaka 1984 Tanzania iliziweka haki za binadamu katika Katiba kufuatia marekebisho ya Katiba namba 5.

## Haki za msingi za binadamu

- Binadamu wote wanazaliwa huru na ni sawa kwenye suala la utu na haki.
- Kila mmoja ana fursa ya kupata haki na uhuru bila kutofautisha kabila, rangi, jinsi, lugha, siasa au maoni mengine, taifa au jamii anapotoka, mali, kuzaliwa au hadhi nyingine.
- Kila mmoja ana haki ya kuishi, uhuru, na usalama.
- Hakuna atakayefanywa mtumwa wala mtwana.

- Hakuna atakayeteswa au kufanyiwa ukatili, unyama au kudhalilishwa.
- Kila mmoja ana haki ya kutambuliwa kila mahali kama binadamu mbele ya sheria.
- Binadamu wote ni sawa mbele ya sheria na wana haki ya kulindwa na sheria bila ubaguzi.
- Kila mmoja ana haki ya kupata suluhisho sahihi kwa vitendo vinavyokiuka haki za binadamu.
- Kila anayeshitakiwa kwa kosa linalostahili adhabu bado kisheria atakuwa hana hatia hadi itakapothibitishwa kuwa ana kosa.
- Hakuna atakayeingiliwa bila ridhaa yake kwenye mambo yake ya siri, familia, nyumbani au mawasiliano.
- Kila mmoja ana haki ya kutembea na kuishi ndani ya mipaka ya nchi yake.
- Ndoa itafungwa pale tu ambapo mwanamke na mwanamume watakuwa wamekubaliana kufunga ndoa.
- Kila mmoja ana haki ya kumiliki mali.
- Kila mmoja ana haki ya uhuru wa mawazo, dhamira na kuabudu.
- Kila mmoja na haki ya kutoa mawazo na kauli / kujieleza.
- Kila mmoja ana haki ya kushiriki kwenye mikutano na umoja ulio halali.
- Kila mmoja ana haki ya kushiriki katika serikali ya nchi yake.
- Kila mmoja, kama sehemu ya jamii, ana haki ya kupata hifadhi ya jamii.
- Kila mmoja ana haki ya kufanya kazi, uhuru wa kuchagua ajira, masharti/taratibu za ajira ambazo zinalinda maslahi na ajira yake.
- Kila mmoja ana haki ya kupata malipo sawa na kazi aliyofanya.
- Kila mtu anayefanya kazi ana haki ya malipo ya haki.
- Kila mmoja ana haki ya kuunda au kujiunga na vyama vya wafanyakazi.
- Kila mmoja ana haki ya kupumzika na kustarehe.

- Kila mmoja ana haki ya kuishi maisha yanayofaa na yanayotosheleza kwa afya yake na ya familia yake.

- Akina mama na watoto wana haki ya kupata matunzo na misaada maalumu.
- Kila mmoja ana haki ya kupata elimu.

- Kila mmoja ana haki ya kushiriki katika shughuli za kiutamaduni wa jamii yake.

## Haki za makundi maalumu

Hapa ijulikane ya kuwa katika jamii kuna wanajamii ambao kutokana na sababu za umri (mdogo au mkubwa), mfumo dume au ulemavu, imepelekea waangaliwe kama kundi maalumu. Hawa ni pamoja na wazee, wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

Hii ni kutokana na hali halisi ya mfumo wa kijamii na kisheria ambao haujawapa nafasi sawa katika jamii kama ambavyo imeainishwa kikatiba na katika mikataba ya kimataifa iliyoridhiwa.

Pia kumekuwepo na mabadiliko katika mifumo ya kijamii ikilinganishwa na hali halisi ilivyokuwa miaka iliyopita. Mifumo ya kisasa ya maisha imeacha pengo la nani hasa ana jukumu la kutunza, kulea, kulinda ama kuhudumia makundi haya maalumu.

Makundi maalumu yapo katika hali ya uduni ya kuweza kunyimwa haki zao za msingi kama zilivyotajwa kutokana na hali iliyowapelekea wao kuwa maalumu.

Uduni huu huwaweka katika nafasi ya kupata madhara zaidi kama umasikini au hata kunyimwa haki ya kurithi, kutumia au kumiliki mali walizozichuma.

Hii inatokea kwa sababu mara nyingi haki hizi huwa katika mikondo au mikono ya watu ambao hawaoni umuhimu wa kuwapatia watu duni haki zao na kuwaacha waendelee kuwa duni zaidi.

Hii ni pamoja na sheria na sera mbali mbali ambazo zinatakiwa kubadilishwa ili kutilia mkazo usawa na haki za binadamu, pamoja na watekelezaji wa sheria ambao wamelelewa na kukuzwa katika mfumo dume ambao kuna wakati hauwaachii wakatenda haki kwa makundi maalumu. Ni katika utaratibu huo Umoja wa Mataifa ulitamka haki za msingi za wazee mwaka 1999.

## Haki za msingi za wazee

### Uhuru:

Wazee

- Wapate chakula cha kutosha, makazi, mavazi, maji safi, na huduma za afya. Vitu hivi vitapatikana kutokana na kipato kuongezeka, jamii kutoa msaada na wazee wenyewe kujihudumia.
- Wapate nafasi ya kuajiriwa, kujiajiri au shughuli nyingine ya kujipatia kipato.
- Wapate uhuru wa kuamua ni lini wapumzike kufanya kazi nzito za kuajiriwa/kujiajiri.
- Wapate elimu na mafunzo wanayohitaji ili kuboresha maisha yao.
- Waishi katika mazingira ambayo ni salama na ambayo wanayapendelea.
- Waishi katika nyumba zao kwa muda mrefu kadiri inavyowezekana.

### Kushiriki:

Wazee

- Waendelee kuwa sehemu ya jamii na kushirikishwa kikamilifu katika kuunda na kutekeleza sera zinazogusa maisha yao na pia kubadilishana ujuzi na vijana.
- Wapate nafasi ya kutoa huduma kwa jamii kulingana na ujuzi, stadi, upendeleo na uzoefu wao.
- Waweze kuunda vikundi, mabaraza na umoja wao.

### Matunzo:

Wazee

- Wanufaike na huduma zinazotolewa na familia, jamii zinazohusu matunzo, usalama kulingana na jamii zinazohusika.
- Wapate huduma bora ya afya ili waboreshe afya zao kimwili na kiakili.
- Wapate huduma za kijamii na kisheria ili waweze kujitegemea, kuwa na amani na utulivu na matunzo wanayoyahitaji.
- Wapate huduma ya makazi yenye usalama na huduma nyingine za kijamii.
- Wapate heshima, wawe na nafasi ya kuamini wanavyotaka, wawe na faragha na waweze kuamua kuhusu aina ya matunzo wanayohitaji.

### Utimilifu:

Wazee

- Wapate nafasi ya kujiendeleza kulingana na uwezo wao.

- Wapate nafasi ya kujijenga kielimu, kiutamaduni, kiroho na kiburudani.

### Heshima:

Wazee

- Wapate heshima, usalama na wasinyanyaswe kiakili wala kimwili.

- Watendewe haki bila kujali umri, jinsia, rangi, kabila, ulemavu au umaskini wao.

- Wathaminiwe kulingana na utu wao na siyo vinginevyo.

## Sheria na haki za binadamu

Kwa kuwa watu hupenda kuishi wapendavyo, wakati mwingine bila kujali maslahi au usalama wa wengine, sheria hutungwa ili kutoa mwongozo na kuwarekebisha watu wanaokiuka taratibu zinazokataza mtu kumuudhi, kumdhurumu au kumnyanyasa mwenzake.

Kwa kifupi sheria za nchi huendana na misingi ya haki za binadamu. Haki za binadamu zinaweka bayana kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria.

Kipimo cha sheria iliyo bora ni ile inayofuata haki za binadamu na kuna utaratibu maalumu uliowekwa kusimamia ulindwaji na utekelezaji wa sheria

# MAHAKAMA ZA TANZANIA

## Maana ya mahakama

Mahakama ni chombo cha kiserikali ambapo sheria hutafsiriwa na kuonyesha maana yake halisi na kutoa hukumu au agizo. Mahakama ni sehemu ya kuheshimiwa na yenye kuhitaji utulivu mkubwa.

Kila mtu anapokuwa mahakamani anatakiwa kuwa makini na mwangalifu kwa yale ambayo ataamua kuyasema. Inatakiwa mtu atoe maelezo yanayoeleweka. Vinginevyo mtu anaweza kupoteza haki yake au ya yule anayemtolea ushahidi. Ni vema ikizingatiwa kuwa kutojua sheria si kinga mahakamani.

Hata hivyo hakuna sababu ya kuogopa mahakama kwani ni sehemu yenye ulinzi na usalama wa kutosha na ndipo mahali haki inapotendeka. Mtu yeyote ana haki ya kufika mahakamani na kusikiliza kesi zinazosikilizwa katika mashauri ya wazi.

## Mfumo wa mahakama Tanzania

Tanzania ina mahakama mbalimbali ambazo zimewekwa kisheria. Mfumo wa mahakama uliowekwa unawawezesha raia kufika mahakamani wanapokuwa na shauri lolote.

Pia mfumo huo unawahakikishia raia kupewa haki kwa kupitia mahakama hizo. Mfano, mtu asiporidhika na uamuzi wa mahakama ya ngazi moja anaweza kwenda mahakama ya ngazi ya juu yake.

### 1. Mahakama za mwanzo

Mahakama za mwanzo ni mahakama za chini katika utaratibu wa mahakama za Tanzania. Mahakama hizi hufunguliwa katika kila wilaya na uwezo wa mahakama hizi huishia ndani ya wilaya husika.

Mahakama za mwanzo zina kazi nyingi kwani hapa ndipo haki inatakiwa kutendeka na watu walio wengi hufikia mahakama hizi. Pia gharama zake ni ndogo ukilinganisha na mahakama nyingine za juu.

Zingatia:

❖ Mahakama za mwanzo hukamilishwa na hakimu mmoja pamoja na wazee wa baraza wasiopungua wawili.

❖ Mara zote hakimu katika mahakama hizi hutakiwa kisheria kukaa na kushauriana na wazee wa baraza wakati wa kutoa maamuzi.

- Maamuzi yoyote yasiyowahusisha wazee wa baraza katika mahakama za mwanzo ni batili.

## 2. Mahakama za wilaya

Mara zote mahakama za wilaya zinakuwa katika makao makuu ya wilaya. Utaratibu wa mahakama hizi si tofauti sana na ule wa mahakama za mwanzo.
Tofauti mojawapo ni kuwa katika mahakama hizi kuna mashauri ambayo husikilizwa faragha (in chambers) na yale ambayo husikilizwa wazi.

Zingatia:

- Mahakama za wilaya huongozwa na hakimu wa wilaya. Mahakimu katika mahakama hizi waweza kuwa zaidi ya mmoja, kutegemea na jinsi watakavyokuwa wameongozwa na mahakama za juu.

- Katika mahakama hizi, si kawaida kuwa na wazee wa baraza isipokuwa kwa kesi zinazohusu sheria za kimila na sheria za kiislamu. Wazee hawa hutumika kumshauri hakimu.
- Mahakimu wa mahakama hizi hawawajibiki kukubaliana na ushauri wa wazee wa baraza iwapo wataona ushauri huo unakiuka haki za binadamu, lakini mahakimu watatakiwa kuandika sababu za kukataa ushauri huo.

## 3. Mahakama za hakimu mkazi

Hizi ni mahakama zinazoanzishwa kwa uamuzi wa Jaji Mkuu kufuatana na sheria inayotumika wakati huo, na hufanya kazi katika maeneo ambayo Jaji Mkuu ameyabainisha.

Zingatia:

- Mahakama hizi huongozwa na hakimu mkazi na utaratibu wa mahakama hizi si tofauti sana na ule wa mahakama za wilaya.

## 4. Uwezo wa mahakama za wilaya/hakimu mkazi

Mahakama hizi zina uwezo wa kupokea rufaa toka mahakama za chini yake. Pia zinaweza kupokea shauri lolote jipya kulingana na sheria iliyopo.

## 5. Mahakama kuu ya jamhuri ya muungano

Hii ndiyo mahakama kuu ya Tanzania yenye uwezo wa kusikiliza kesi zote za madai na jinai. Mahakama hii huongozwa na Jaji Mkuu na Majaji wengine wasiopungua 15.

Zingatia:

- ❖ Kwa kawaida mahakama hii huongozwa na Jaji mmoja wakati wa kusikiliza rufaa. Lakini wakati wa kesi yoyote ya jinai, kesi husikilizwa pamoja na wazee washauri wa mahakama wawili au mmoja.

- ❖ Hata hivyo Jaji hafungwi na ushauri wa wazee wa mahakama endapo ataona haki haitatendeka iwapo ataufuata ushauri huo.

Uwezo wa mahakama kuu

Mahakama hii haina kikomo cha uwezo wake katika kesi zote za madai na jinai. Pia mahakama kuu ndiyo kiungo kikuu cha kuangalia na kuhakikisha kuwa haki inatendeka katika mahakama zote.

Mahakama hii imepewa uwezo wa kikatiba kusikiliza masuala yote yahusuyo taratibu za kisheria zinazotumika nchini Tanzania bila kuathiri mamlaka ya mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

Mahakama hii hupeleka rufaa zake Mahakama ya Rufaa Tanzania.

Mahakama hii inao uwezo wa kuitisha na kupitia usahihi wa faili au kurudia vipengele fulani katika shauri lolote toka mahakama ya wilaya au hakimu mkazi, kulingana na jinsi ambavyo itaona inafaa.

## 6 . Mahakama ya rufaa ya Tanzania

Mahakama ya rufaa ilianzishwa mwaka 1979 baada ya kufutwa kwa mahakama ya rufaa ya Afrika Mashariki.

Zingatia:

- ❖ Mahakama ya rufaa ndiyo mahakama ya juu kuliko zote hapa nchini. Mahakama hii ina uwezo wa pekee na usio na mipaka katika kesi zote za madai na jinai.

- ❖ Hata hivyo, kama ilivyo katika mahakama za ngazi nyingine zilizoelezewa hapo juu, mahakama hii haina uwezo wa kushughulikia kesi zinazohusu masuala ya Muungano wa Tanzania, ambayo huamuliwa na mahakama maalumu ya katiba, ambayo huwa na kazi hiyo pekee.
- ❖ Mahakama ya rufaa haina uwezo wa kupokea mashauri mapya, yenyewe hupokea tu mashauri yanayokuja kama rufaa kutoka mahakama kuu.

- ❖ Kesi inapoamuliwa kwenye mahakama za rufaa itakuwa ndiyo imefikia mwisho na hakuna rufaa nyingine tena katika mfumo wa mahakama za Tanzania.

# TARATIBU ZA MAHAKAMA

## Kesi za madai

Kesi za madai ni zile ambazo zinahusiana na mahusiano ya kawaida ya watu, k.m. kesi za ndoa, mashamba, mikataba n.k.

## Utaratibu wa sheria katika kesi za madai

Kawaida katika kesi za madai serikali haijihusishi sana. Ndiyo maana yeyote anayefungua kesi ya madai mahakamani hulipa fedha kulingana na gharama za madai au mkataba wake.

Mahakama hutegemea maelezo ya mdai na mdaiwa kwani ndiyo wanaojua mazingira yote ya kesi yao. Hakimu huwa ni msikilizaji na mwandishi wa yale yanayoelezwa. Polisi huwa haijihusishi na upelelezi wowote.

Iwapo itabidi kumuweka wakili, gharama za kumlipa hulipwa na wahusika, siyo serikali. Pia katika kesi hizi wahusika hawawezi kupelekwa moja kwa moja gerezani.

Ni nia ya serikali kuhakikisha kwamba kesi hizi zinaisha haraka na kutoa mwanya kwa wananchi kufanya shughuli za kiuchumi zaidi kuliko kuendelea na kesi.

Katika kesi za madai huwa hakuna kifungo wala faini. Kinachotolewa huwa ni fidia tu pamoja na kulipa gharama ambazo aliyeshinda alizigharimia katika kesi nzima.

## Mwenendo wa kesi katika kesi za madai

Kabla ya kufungua kesi ya madai mahakamani unatakiwa kutuma barua ya madai kwa mdeni wako au mdaiwa. Barua hiyo inatakiwa kuwa wazi katika maeneo yafuatayo:

- Ionyeshe jina la mdai na mdaiwa.

- Ionyeshe/itaje madai halisi (kiasi au vinginevyo).

- Itoe muda wa kulipa deni/kutimiza wajibu huo.

- Ionyeshe wazi kuwa endapo mdaiwa hatatimiza wajibu wake kwa muda huo ulioelezwa hatua za mahakama zitafuatwa.

Kesi zote ambazo siyo za kufunguliwa mahakama kuu hufunguliwa pale kinachogombewa katika mgogoro kilipo au anapokaa mdaiwa.

*Mfano:* Kama kinachogombewa ni shamba ambalo lipo Morogoro na mlalamikiwa yupo Dodoma, itabidi kesi ifunguliwe Morogoro shamba lilipo au Dodoma alipo mlalamikiwa.

Wakati wa kesi mdai na mdaiwa hutakiwa kuwa na mashahidi wao na ni kwa gharama zao.

Mlalamikiwa (mdaiwa) asipofika mahakamani siku, saa na mahali palipopangwa mara kadhaa, hukumu huweza kupitishwa wakati yeye hayupo.

Hata hivyo akijitetea kuwa hakupata wito (samansi), au atathibitisha kuwa kulikuwepo na sababu za msingi zilizomzuia kuhudhuria na utetezi wake ukikubaliwa wanaweza kuruhusu hukumu isomwe wakati yeye yupo siku nyingine.

Mlalamikaji (mdai) au wakili wake asipofika mahakamani kama ilivyopangwa bila sababu, kesi hiyo itafutwa isipokuwa tu pale ambapo mdaiwa atakiri kutolipa au kutimiza wajibu ambao ndiyo chanzo cha mgogoro.

## Kesi za jinai

Makosa ya jinai ni yale yanayotendwa dhidi ya dola na yameorodheshwa katika kitabu cha kanuni ya adhabu ambapo adhabu yake imetayarishwa na dola.

Makosa ya jinai yapo ya aina nyingi mfano makosa yanayomhusu binadamu, makosa ya zinaa, makosa yanayohusu mali n.k.

## Utaratibu wa sheria katika kesi ya jinai

Katika kesi za jinai wakili wa serikali humwakilisha mlalamikaji bila gharama yoyote kwa sababu makosa yenyewe ni dhidi ya raia ambao dola ina wajibu wa kuwalinda.

Ndiyo maana mlalamikaji katika kesi hizi huwa Jamhuri kupitia kwa mwanasheria wa serikali, polisi kama chombo cha dola au mwendesha mashtaka ambaye ndiye hutoa maelezo. Hapa raia aliyetendewa kosa huhesabika kama shahidi namba moja.

Mtu yeyote anayehisi kutendeka kwa kosa anaweza kuripoti shauri hilo kwa polisi ambao watafanya utafiti na kumkamata mtuhumiwa ili kumfikisha mahakamani kwa kosa alilotenda.

Pia katika kesi za jinai mtu yeyote anayeamini kuwa kosa la jinai limetendeka anaweza kutoa taarifa moja kwa moja kwa hakimu ambapo hakimu ataandika maelezo hayo.

Mtu anayetiliwa mashaka anaweza kukamatwa mara baada ya upelelezi kukamilika au kabla upelelezi haujakamilika kutegemeana na kosa analoshitakiwa nalo.

Katika kesi za jinai anayethibitika kuwa na kosa huweza kuhukumiwa faini, kifungo au adhabu zote mbili.

Kusikilizwa kwa kesi ya jinai huhitaji kuwepo kwa mashahidi kutoka kwa mlalamikaji na mtuhumiwa. Kitendo cha shahidi kutofika mahakamani ni kosa la jinai, labda ukitolewa ushahidi kuwa samansi haikumfikia shahidi huyo.

Mtu yeyote anayeaminika kuwa ana ushahidi wa muhimu ambao utaiwezesha mahakama kutoa haki atalazimishwa na mahakama kutoa ushahidi huo au kuwasilisha taarifa muhimu alizonazo kuhusu kesi hiyo.

Endapo mtu huyo hataweza kufika mahakamani mpaka alazimishwe, amri ya kukamatwa kwake itatolewa ili akamatwe na kuja kutoa hizo taarifa au nyaraka za ushahidi.

Endapo mlalamikaji atashindwa kufika mahakamani baada ya kuhakikisha kuwa alipewa samansi wakati unaofaa, alijua tarehe na mahali kesi itakaposikilizwa, mahakama inaweza kufuta kesi dhidi ya mtuhumiwa.

# SHERIA YA USHAHIDI MAHAKAMANI

Ushahidi huhusu mambo yote mtu anavyojua, alivyoona, alivyonusa, alivyogusa, alivyoonja na alivyojaribu. (Ushahidi huhusu maonjo au hisia zote za binadamu). Pia ushahidi unaweza kwenda zaidi ya maonjo ya binadamu kwa mfano maoni ya wataalamu k.m. mtaalamu wa maandishi, madaktari, anayepima maiti, mtaalamu wa kemia, mtaalamu wa vidole n.k.

## Aina za ushahidi

### *Ushahidi wa wazi*

Ushahidi huu ni wa moja kwa moja ambao mara zote hutolewa na mtu ambaye alishuhudia mwenyewe tukio.

***Mfano:*** Mimi nilikuwa na mlalamikaji pale nyumbani kwake, nikamwona mlalamikiwa anakuja na ghafla akaanza kumpiga makofi mlalamikaji.

Huu ndiyo ushahidi unaokubalika mahakamani kwa kuwa anayeutoa anayo maelezo ya kutosha na ya uhakika kuhusu tukio husika.

### *Ushahidi wa kimazingira*

Huu ni ushahidi unaotolewa na mtu ambaye hakushuhudia tukio moja kwa moja. Ni ushahidi wa kushuku kutokea kwa tukio kutokana na mazingira yanayolizunguka tukio lenyewe.

***Mfano:*** *Ninaamini Koko ndiye aliyeiba mbuzi kwani mbali na yeye kukana kuwepo kwa mbuzi nyumbani kwake hiyo jana, mimi nilisikia mlio wa mbuzi nyumbani kwake usiku wa manane na leo tumeona samadi na manyoya ya mbuzi pamoja na damu jikoni kwake.*

Mara nyingi mahakama huwa makini wakati wa kupokea ushahidi huu kama ushahidi kamili kwa sababu ni rahisi kughushi au kutoa ushahidi usio wa kweli kwa njia hizo.

Inawezekana mtoa ushahidi akawa na visa na mtuhumiwa. Ili ushahidi huo ukubalike ni lazima usaidiwe na ushahidi mwingine utakaoendelea kuuthibitisha.

### *Ushahidi wa kusikia*

Huu ni ushahidi unaotolewa na mtu ambaye hakuwa kwenye tukio, ila alisikia kwa watu wengine wakisema hivyo. Mara nyingi ushahidi huu haukubaliki mahakamani kwa sababu zifuatazo:

- Aliyeshuhudia tukio likitendeka na baadaye kutoa maneno hayo hayupo na hivyo hawezi kuapishwa.

- Ushahidi hauwezi kuulizwa maswali kwani mtu ambaye anautoa mahakamani siye aliyeshuhudia tukio likitendeka.

- Ni rahisi ushahidi huo kupotoshwa kwani aliyesikia maneno hayo anaweza kuongeza chumvi kulingana na matakwa yake.

### *Ushahidi wa maandishi*

Huu ni ushahidi ambao hutolewa kulingana na maandishi yaliyopo katika karatasi fulani. Ushahidi huu nao unakubalika ili mradi maandishi hayo yasiwe yamenakiliwa na yasiwe maandishi kivuli.

Hata hivyo mahakama yaweza kukubali vivuli vya nyaraka zozote ambazo kisheria hazitakiwi kusomwa na watu wote, mfano nyaraka za serikali.

### *Ushahidi wa kitaalamu*

Huu ni ushahidi unaotolewa na wataalamu wa mambo mbali mbali k.m. wataalamu wa maandishi, viumbe n.k.

Ushahidi huu hata hivyo si lazima ukubaliwe kuwa sehemu ya hukumu ya kesi ila ni maoni ambayo yanatoa mwongozo wa kufanikisha ugunduzi wa kitu fulani. Kukubalika kwa ushahidi huu hutegemea jinsi mahakama itakavyoona ni haki na halali.

### Nani anaweza kutoa ushahidi

Mtu yeyote mwenye umri unaokubaliwa kisheria, na mwenye akili timamu aweza kutoa ushahidi juu ya jambo lolote.

Makundi ambayo ushahidi wao hutolewa kwa utaratibu maalum wa kisheria ni:

- Mtoto ambaye ushahidi wake lazima usaidiwe na ushahidi mwingine endapo mahakama itapenda kufanya hivyo.

- Mahakimu na Majaji ambao hutoa ushahidi pale tu inapokuwa lazima. Vinginevyo hawawezi kulazimishwa kutoa ushahidi mahakamani kuhusu kazi yao wawapo mahakamani.

Kwa sheria ya sasa mke au mume wa mshtakiwa anaweza kutoa ushahidi mahakamani. Pia anaweza kulazimishwa kutoa ushahidi dhidi ya yeyote anayetuhumiwa hata kama ni mke

au mume wake.

Kwa hali yoyote ile, hakuna anayelazimishwa kutangaza mawasiliano yoyote ya siri aliyoyafanya na wakili wake kuhusu kesi yake.

### *Ushahidi unaokubalika mahakamani*

Ushahidi unaokubalika mahakamani ni ule unaopelekea kuthibitisha kutendeka au kutotendeka kwa kosa linalodaiwa kutendwa. Ushahidi wowote unaoeleza jambo lililo tofauti na kosa haukubaliki mahakamani.

Shahidi anatakiwa kuongea kwa ufasaha na uhakika ili kuifanya mahakama iamini maneno anayoyasema. Pia anatakiwa kuwa mtulivu na kutokuwa na hasira.

Ni makosa kutoa ushahidi wa uongo.

# RUFAA

Rufaa ni ombi la kisheria la kutaka kesi au shauri husika liendelee kusikilizwa katika mahakama nyingine ya juu kwa sababu ya makosa au mapungufu fulani ya kisheria.

Rufaa ni haki ya kila upande wa wahusika katika kesi. Aliyeshinda anaweza kuomba rufaa kwa kutoridhishwa na adhabu iliyotolewa kwa aliyeshindwa; na aliyeshindwa anaweza kuomba rufaa kwa kutoridhishwa na hukumu au vipengele vya kisheria vilivyotumika katika mwenendo wa kesi.

Nia ya kukata rufaa huelezwa mara tu baada ya hukumu kusomwa na adhabu kutolewa katika kesi za jinai.

Muda wa kukata rufaa ni siku 30 tangu tarehe ya hukumu. Lakini mara nyingi sana nakala za hukumu huchelewa kutolewa na kusababisha wahusika kuchelewa kukata rufaa. Hivyo utaratibu unaotumika sasa ni kuwa sababu za rufaa hupelekwa katika muda wa siku 30 baada ya kutolewa kwa nakala ya hukumu.

## Mwenendo wa rufaa

Kwa kawaida mwomba rufaa halazimiki kuwepo wakati wa kusikilizwa kwa rufaa yake isipokuwa kama atapenda mwenyewe kufanya hivyo. Kama hatapenda itabidi awe ameonyesha kwenye karatasi ya rufaa.

Katika mahakama za wilaya, kwa kesi za jinai, mkata rufaa hufika peke yake na upande wa Jamhuri hauwakilishwi na mtu.

Katika kesi za madai wahusika wote hufika, lakini mwomba rufaa aweza kuacha kufika kwa taarifa. Katika mahakama kuu, kwa kesi za jinai, wahusika wote huhudhuria.

Uamuzi unaotolewa baada ya rufaa kusikilizwa huwa ni kuunga mkono hukumu iliyokuwa imetolewa au kuifuta kabisa hukumu hiyo na kutoa amri ya kesi nzima kusikilizwa upya.

Kama rufani hiyo ilihusu adhabu, basi adhabu hiyo inaweza kupunguzwa au kuongezwa kutegemea na ukubwa wa kosa.

# DHAMANA

Dhamana ni ruhusa inayotolewa kwa ahadi/malipo ili mtuhumiwa atolewe/asiwekwe rumande wakati kesi yake inaendelea kusikilizwa.

Katika hali ya kawaida kila mshitakiwa ana haki ya kupewa dhamana kwani kisheria mshitakiwa atakuwa hana hatia mpaka wakati ule mahakama itakapothibitisha kuwa ana hatia.

Pia dhamana hii ipo ya aina mbili;

- ❖ Dhamana inayotolewa kituo cha polisi:- Aina hii ya dhamana hutolewa kwa mshitakiwa akiwa kituo cha polisi kwa makosa yanayoruhusiwa kutolewa dhamana.

- ❖ Dhamana inayotolewa mahakamani:- Aina hii ya dhamana hutolewa mahakamani kwa makosa yale yanayoruhusiwa kutolewa dhamana.

***Zingatia :***
Dhamana haitolewi kwa kwa makosa mazito  kama vile, mauaji na uhaini.

Mshitakiwa anaweza kunyimwa dhamana na mahakama iwapo:

- Mahakama itatilia shaka uwezekano wa mshitakiwa kuwa amefika mahakamani wakati kesi inaendelea.

- Mahakama itaona uwezekano wowote ule wa mshitakiwa kutenda kosa jingine pindi atakapopewa dhamana.

- Mahakama itaona uwezekano wa mshitakiwa kuingilia upepelezi wa kesi kwa kuwarubuni mashahidi wanaopelekwa mahakamani.

- Mahakama itatilia shaka usalama wa mshtakiwa atakaporudi kwenye jamii.

- Mahakama itazingatia uzito wa kosa lenyewe na adhabu inayoweza kutolewa na kuona kuwa ni dhahiri mshitakiwa akipewa mdhamana atatoroka kwani anajua kuwa atakapotiwa hatiani adhabu yake ni kubwa.

***Mfano:*** *Mtu aliyeshitakiwa kwa kosa la kuua kwa kukusudia anajua kuwa akitiwa hatiani adhabu yake yaweza kuwa ni kifo*

Dhamana hutolewa wakati mshtakiwa anapoletwa mahakamani. Mtu/watu wa kumdhamini mshtakiwa hupewa masharti na mahakama.

Mtu anayemwekea mdhamana mshtakiwa, anatakiwa kuhakikisha mshtakiwa hatoroki na anahudhuria mahakamani kama ilivyopoangwa. Iwapo atatoroka, mdhamini hupewa muda na mahakama wa kumtafuta na kumfikisha mahakamani.

Asipompata mshitakiwa mdhamini hulazimika kulipa gharama ambayo waliweka mahakamani kama dhamana.

Kulipa gharama hiyo huwa siyo mwisho wa kesi ya mshtakiwa. Mshtakiwa akionekana kesi yake huendelea.

HelpAge International Tanzania
134 Migombani Street, Regent Estate, Mikocheni
P.O. BOX 9846 Dar es Salaam Tanzania
Tel: +255 22 2774796/2700169
Fax: +255 22 2775894

Email: haitz@helpagetz.org
Website: www.helpage.or

Copyright © HelpAge International 2014
Registered charity no. 28810